
**CAPITAL MARKETS AND SECURITIES AUTHORITY**

**MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA**

# MTANZANIA JIHADHARI NA UPATU HARAMU “NI HATARI KWA MAENDELEO YAKO NA TAIFA KWA UJUMLA”



***Jifunze kusema “hapana” na jihadhari na matapeli wanaoahidi watu Kuvuna pesa nyingi kirahisi. Epuka kupoteza pesa ya jasho lako, epuka upatu haramu***




Pamoja na tahadhari kutolewa kwa njia ya Magazeti, matangazo na taarifa kwa umma kuhusiana na hatari ya kushiriki michezo ya upatu haramu, jamii ya watanzania imekuwa bado inajihusisha na upatu haramu. Kijarida hiki kimeandaliwa ili kuuwezesha umma uweze kutambua na kujihadhari na upatu haramu.

**NINI MAANA YA UPATU HARAMU?**

Upatu haramu ni mpango wa kuchangisha fedha unaoendeshwa na mtu au kikundi fulani cha watu kwa ahadi ya kuwapatia wachangiaji kiasi kikubwa cha faida katika kipindi kifupi. Ili mpango uweze kuendelea washiriki wanatakiwa kujiunga kwa wingi sana, mipango hii ni lazima ife (ianguke) katika kipindi kifupi kwa kuwa kuna ukomo wa kupata washiriki wapya. Malipo kwa washiriki hutegemea:-

- ✓ Kuongezeka kwa idadi ya washiriki katika mpango, au
- ✓ Kuongezeka kwa michango inayotolewa na washiriki katika mpango.

**Aina za Upatu Haramu**.

- ✓ Upatu haramu wenye malengo ya kutoa huduma baada ya kupokea michango kutoka kwa washiriki mbalimbali. Mamia hushawishika

kuchangia kwa ahadi ya kupatiwa huduma bure kama kulipiwa ada ya shule, kujengewa nyumba. Mara nyingi washiriki hudanganywa kuwa kuna wafadhili watakaogharamia huduma hizo.

- ✓ Upatu haramu kwa njia ya barua ikutakayo upeleke kiasi fulani cha pesa kwa watu waliotajwa kwenye hiyo barua halafu wewe uongeze jina lako kwenye hiyo barua.
- ✓ Kuna upatu haramu inayoambatana na uuzaji wa bidhaa. Washiriki hushawishiwa kujiunga kwa kutoa kiasi fulani cha pesa kama kiingilio na kisha kupatiwa bidhaa zenye thamani kidogo kuliko kiingilio alichotoa. Mshiriki hulazimika kununua bidhaa kwa bei ya juu kutoka kwao kila mwezi na kutafuta washiriki wapya ili wajiunge na mtandao huo. Mipango inayoambatana na uuzaji wa bidhaa ni ya kitapeli na wizi kwasababu bidhaa hizo:
    - Huuzwa kwa bei ya juu sana ili kuwezesha upatu haramu kulipa malipo kwa washiriki wake;
    - bidhaa hizo kwa kawaida huwa hazihitajiki sana kwa matumizi ya kawaida na hivyo kutokuwa na soko.

**Jinsi watu wanavyoghilibiwa kujiunga na upatu haramu:-**

- ✓ Ahadi kuwa fedha itaongezeka maradufu au zaidi kwa muda mfupi;
- ✓ Ahadi ya kupewa asilimia ya faida isiyokuwa ya kawaida, wakati mwingine mpaka asilimia mia mbili na zaidi;
- ✓ Simu na barua zisizotarajiwa;
- ✓ Taasisi inayoshawishi au watendaji wake wakuu kuhusishwa na dini na hivyo kuwa rahisi kurubuni waumini wao;
- ✓ Waanzilishi wa upatu haramu ni wazuri sana wa kughilibu akili za washiriki kisaikolojia. Huwa wanafanya mikutano ya kushawishi washiriki wapya kwa ufanisi na ushawishi kwa kutoa ahadi nono na hivyo kumfanya mshiriki mtarajiwa kuwa na wakati mgumu kukataa vishawishi vya kujipatia pesa kwa urahisi;
- ✓ Waendesha mpango kuonyesha orodha ya watu mashuhuri kijamii na kisiasa ambao wanadaiwa kushiriki upatu haramu kwa mafanikio;
- ✓ Washiriki kutopewa muda wa kutosha kutafuta ushauri kwa maelezo kwamba watakosa bahati.

**Ahadi ya malipo makubwa mara nyingi huwa na masharti kuwa mshiriki yapasa:**

- ✓ ashawishi wengine kujiunga na mpango wa upatu haramu, au
- ✓ aongeze idadi ya washiriki wa mpango wa upatu haramu, au
- ✓ kuwapo kwa ongezeko la mchango au uwekezaji wa washiriki

## MADHARA YA UPATU HARAMU

Uzoefu kutoka nchi mbalimbali ambazo zimekabiliwa na tatizo la upatu haramu, umedhihirisha kwamba mipango hiyo inaweza kuleta madhara ya kiuchumi, kijamii na pengine kisiasa kama inavyoelezwa hapa chini:

**Madhara ya kiuchumi**

- ✓ Watu huondoa mitaji kutoka kwenye shughuli za kiuzalishaji na huzielekeza kwenye upatu haramu usiokuwa na tija kiuchumi;
- ✓ Waweza kusababisha uhamishaji wa mitaji kwenda nje ya nchi (capital flight) na hivyo kuzorotesha shughuli za ndani na kusababisha upungufu wa fedha za kigeni..
- ✓ Watu walioathiriwa na upatu haramu hugeuka kuwa mzigo mzito kwa serikali na jamii iliyowazunguka kutokana na kutomudu gharama za maisha.
- ✓ Wananchi huzama katika lindi la mawazo ya kuvuna mapesa tu na hivyo kutoshiriki ipasavyo katika shughuli za uchumi kama kilimo, viwanda na biashara.
- ✓ Kusababisha kuanguka kwa SACCOS, kudidimiza mabenki, kushindwa kurejesha mikopo kwenye mabenki pindi mipango hiyo inapokufa, kusababisha mfumuko wa bei, nk.
- ✓ Washiriki wengine hukopa ili kushiriki kwenye michezo hii, kuanguka kwa michezo hii huwaacha wakiwa hawana uwezo tena wa kulipa mikopo hiyo na hivyo kuweza kufilisiwa ili kulipia madeni na hivyo kuathirika na kuadhirika kwa kiwango cha kutisha.

**Madhara ya kijamii**

- ✓ Kuanguka kwa upatu haramu hii yaweza kuleta machafuko na kutoelewana miongoni mwa marafiki, familia na jamii kwa sababu ya kupoteza pesa au mali nyingi.
- ✓ Kuvunjika kwa ndoa za washiriki;
- ✓ Kushindwa kulipia ada ya watoto kutokana na kutumia fedha za familia katika mipango ya upatu na hivyo kuongeza ujinga na umasikini katika jamii.
- ✓ Kufukuzwa kazi na pengine kushitakiwa kutokana na kushindwa kulipa fedha za mwajiri zilizotumika kwenye upatu haramu bila idhini ya mwajiri;

**Madhara ya kisiasa**

- ✓ Kusababisha machafuko ya kisiasa yanayosababishwa na watu kudai fedha zao walizopanda;
- ✓ Jamii hukosa kuiamini serikali yao na hivyo kusababisha uasi dhidi ya serikali. Mfano mmojawapo ni ule wa nchi ya Albania ambako wananchi waliangusha Serikali kwa kushindwa kudhibiti upatu haramu.

**Nini wajibu wa jamii katika kupambana na mipango hii ya upatu haramu?**

- ✓ Toa taarifa kwa mamlaka husika au vyombo vya usalama kama polisi mara moja unapoona dalili za upatu haramu;
- ✓ Wasiliana na mamlaka zinazohusika kama Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana au Benki Kuu ili kufahamu endapo mpango unaotarajia kushiriki umeidhinishwa kuchangisha fedha toka kwa umma;
- ✓ Shiriki kuelimisha wengine wasiojua kuhusu madhara ya upatu haramu ,
- ✓ Epuka kushiriki au kujiunga na mipango ya upatu haramu na

kulinda mali au fedha ulizopata kwa jasho.

- ✓ Watake wanaokushawishi kujiunga wakupatie waraka wa matarajio ili uweze kuusoma na hatimaye kufanya maamuzi kwa makini.

**Zingatia**

- ✓ Umma unapaswa uelewe kuwa ahadi ya malipo yasiyo na ukomo au kulipa malipo manono sana kwa washiriki wote ni jambo ambalo halitekelezeki.
- ✓ Jamii yapaswa itambue kuwa ni vyema kujiweka mbali na upatu haramu, kuliko kuja kulia na kusaga meno pale ambapo mali au pesa zao zitakapoibiwa kitapeli;
- ✓ Kumbuka Mipango ya upatu haramu ni lazima ife, kama sio siku za karibuni basi baadaye. Washiriki wengi, hasa hasa wapya watapoteza pesa zao walizoingiza katiak upatu haramu, na kama ni upatu unaombatana na bidhaa watabakiwa mikononi mwao na bidhaa ambazo bei zake ni kubwa kupindukia zisizouzika sokoni.
- ✓ Mtu yeyote anayecheza au kuchezesha upatu haramu anatenda kosa la jinai anaweza kutozwa faini, kufungwa jela au vyote kwa pamoja.

***Mwananchi tafakari kabla ya kutenda, chukua tahadhari kabla ya hatari, kumbuka kuendesha, kushiriki, kushawishi kushiriki au kuchangia upatu haramu ni kosa la jinai. Kuwa mjanja epuka matapeli.***

**<u>Toa tarifa kwa vyombo vya usalama na mamlaka husika kama:</u>**

**Polisi: Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai: Simu. 0732 999154.**
**Tovuti: www.policeforce.go.tz**

**Benki Kuu ya Tanzania: simu (22) 2233000/20**
**Tovuti: www.bot-tz.org**

**Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana: simu (22) 2114959/61**
**Baru apepe: info@cmsa.go.tz**
**Tovuti: www.cmsa.go.tz**

***Imetolewa na:***

**CAPITAL MARKETS AND SECURITIES AUTHORITY**

**MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA**


**Afisa Mtendaji Mkuu**
**Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana**
**Ghorofa ya 6, Jengo la PPF Tower,**
**Makutano ya Mtaa wa Ohio na Garden,**
**S.L.P. 75713 Dar es Salaam,**
**Simu: +255 22 2114959 / 61**
**Faksi: +255 22 2113846**
**Barua pepe:**
**info@cmsa.go.tz**
**Tovuti: www.cmsa.go.tz**